

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

Simu: 026-2322129
Nukushi: 0256-2322126
Barua pepe: km@michezo.go.tz
Tovuti: www.michezo.go.tz



Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Michezo,
S.L.P 25,
40481 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

**TANZANIA YAJIUNGA TENA UANACHAMA WA SHIRIKISHO LA
KIMATAIFA LA MABARAZA YA SANAA NA UTAMADUNI**

DODOMA, Machi 15, 2023.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Balozzi Dkt. Pindi Chana, (Mb) anawajulisha wadau wa Sanaa na Utamaduni na Watanzania wote kuwa Taifa letu limefanikiwa kujiunga tena uanachama wa Shirikisho la Kimataifa la Mabaraza ya Sanaa na Mashirika ya Utamaduni, (***International Federation of Arts Councils and Culture Agencies - IFACCA***) kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA).

Hatua hiyo ni matokeo mazuri ya kuimarika kwa sifa za Tanzania katika medani ya Diplomasia na Ushirikiano wa Kimataifa hususani katika Sekta ya Sanaa kutokana na uongozi thabiti wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kutokana na Tanzania kujiunga katika Shirikisho hilo, Katibu Mtendaji Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Dkt. Kedmon Mapana anakuwa Mjumbe atayeiwakilisha Tanzania katika Mkutano wa Shirikisho la Kimataifa la Mabaraza ya Sanaa na Mashirika ya Utamaduni ambapo kwa mwaka huu utafanyika jijini Stockholm, Sweden.

Waziri Balozzi Dkt. Pindi Chana, (Mb) amelipongeza Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kwa kuwa mwanachama wa Shirikisho la Kimataifa la Mabaraza ya Sanaa na Mashirika ya Utamaduni jambo litakalosaidia kwa kiasi kikubwa kutoa fursa mbalimbali kwa wasanii wa Tanzania kubadilishana ujuzi, ubunifu, pamoja na kutanua wigo wa soko la maudhui ya kazi za sanaa zinazohitajika kupitia ushirikiano na kuhudhuria makongamano yanayoendeshwa na Shirikisho hilo kila mwaka katika nchi wanachama ikiwemo Tanzania.

Aidha, ameliagiza BASATA liendelee kuimarisha uhusiano na wadau mbalimbali wa maendeleo ya sanaa ndani na nje ya nchi ili kusaidia kutumia kazi za sanaa katika kuhamasisha na kupenyeza ajenda za maendeleo kwa kuwa sekta ya sanaa inaongoza kutoa ajira na kuingiza kipato nchini.

Imetolewa na:-



Aron Msigwa

KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI